OPENER EXAMINATION: TERM 1 2024

# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KIDATO CHA PILI

**SEHEMU YA A INSHA.** **(ALAMA 20)**

Hii ni insha ya hotuba. Vipengele muhimu vya insha ya aina hii viweze kudhihirika.

Sehemu zifuatazo zidhihirike:

1. **Anwani/Kichwa.**

Kichwa kiweze kutaja:

(i) Kuwa ni hotuba

(ii) Hatibu-anayehutubu

(iii) Mada inayozungumziwa.

2. **Utangulizi**

Hatibu husalimu hadhira yake akianzia na wenye vyeo na madaraka ya juu hadi chini kabisa.

Hatibu anaweza pia kudokeza mada ya hotuba.

3. **Mwili**

Hii ndio sehemu ambayo inabeba maudhui ya insha.

Sehemu hii huwa na hoja ambazo huwa zimepangwa kwa kutumia aya.Kila hoja huwa inafafanuliwa ipasavyo.

4. **Hitimisho**

Hii ni sehemu ya mwisho wa hotuba na hatibu hana budi kushukuru hadhira kwa kumsikiliza.

**Maudhui ambayo yanaweza kujitokeza ni kama yafuatayo.**

(i)Wanafunzi kuwa na nidhamu.

(ii)Wanafunzi kuamka mapema ili wapate wakati wa kudurusu.

(iii)Wanafunzi kujiunga na makundi wanapodurusu ili kuinuana.

(iv)Kuepukana na kelele darasani.

(v)Wanafunzi kuzingatia yaliyomo kwenye mtaala.

(vi)Watumie karatasi za mitihani iliyopita wakidurusu.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(vii)Kuuliza walimu maswali wanapolemewa.

(viii)Kuhakikisha wamekamilisha kazi ya ziada wanayoachiwa na walimu.

(ix)Kutolala darasani.

(x)Kuhudhuria mahudhurio yote darasani.

(xi)Kujihusisha na michezo katika shule.

**SEHEMU YA B:UFAHAMU** (ALAMA 15)

1.Anwani/Kichwa. (Alama 1)

Watoto wa mitaani.

Watoto wanaorandaranda mitaani.

2.Vyanzo (Alama 3)

(i) Baadhi ya wazazi kuwa makahaba

(ii) Kuvunjika kwa ndoa.

(iii) Wazazi kuaga dunia.

(iv) Familia masikini kushindwa kutimiza mahitaji ya watoto.

3. Athari za kutengana kwa wazazi. (Alama 1)

Watoto hukosa mihimili na hivyo kushika hamsini zao hadi mitaani kutafuta riziki.

4. Masaibu yanayowapata watoto. (Alama 2)

(i)Hukosa chakula,mavazi na malazi.

(ii)Hawana usalama

5. Watoto wa mitaani ni kero. (Alama 2)

(i)Hupamba miji kwa sura mbaya.

(ii)Hutumia lugha chafu

(iii)Wengine huwa na vitisho

6. Jinsi ya kukomesha (Alama 2)

(i)Wanajamii kuwa waadilifu.

(ii)Kila mwanajamii kutia bidii kutafuta riziki

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(iii)Kupanga uzazi. Kupata watoto mtu anaweza kulea bila usumbufu.

(iv)Watoto mayatima walelewe na jamaa wa wazazi wao

(v)Wasio na jamaa wapelekwe kwenye mashirika ya kuwatunza watoto.

(vi)Walio mitaani wasaidiwe na serikali kupata makao na ajira.

7. Msemo (Alama 2)

(i) Kushika hamsini zao

(ii) Kuaga dunia

(iii) Kutia bidii

8. Msamiati (Alama 2)

(i) Ukahaba- uzinzi/ uasherati/ ukware

(ii) Ajira- kazi

**SEHEMU YA C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

1.(i)Irabu ya nyuma juu viringwa. /u/ (Alama 2)

(ii)Nazali ya midomo /m/

2. Miundo ya silabi (Alama 2)

Muungwana mu-u-ngwa-na

Ki I kkki ki

3.Ukubwa (Alama 2)

Jitu hilo lilibwekewa na jibwa.

4.Kuyakinisha (Alama 2)

Nimeridhika na kazi ya mwanafunzi yule.

5.Matumizi ya kistari kifupi (Alama 2)

(i)Kutenganisha mofimu a-na-li-ma

(ii)Kuonyesha mzizi -refu

-kubwa

Teacher.co.ke
Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

(iii)Kuandika tarehe 7-10-2022

(iv)Kuonyesha kuendelezwa kwa sauti sala-a-lee.

6.Ngeli (Alama 2)

(i)Kipepeo A-WA

(ii)Waraka U-ZI

7. Wale werevu /walituzwa zawadi. (Alama 4)

S----KN(W+V)+KT(T+N)

8.Viambishi (Alama 2)

Kilichopigwa

Ki

li } Viambishi awali

cho

pig } mzizi

w } V iambishi tamati

a

9.Wingi (Alama 2)

Viatu vyetu vilipatikana kwao.

10.(i)Tumefikisha mzigo wake nyumbani.

(ii)Yeye huongea na mfadhili wake ili apate ufadhili zaidi. (Alama 2)

11.Aina za vivumishi (Alama 2)

Changu –kivumishi kimilikishi

Maridadi-kivumishi cha sifa

12.Kunyambua (Alama 2)

(i)Choka (kutendesha) chosha

(ii)Lima (kutendea) limia

13"Nani atamsaidia mtoto huyu?"Penina akauliza (Alama 3)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

14.Shadda

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

Teacher.co.ke

(i)Ka'lamu

(ii)Ba'rabara (shwari) (Alama 2)

15. Zawadi ambazo tulipata zilinunuliwa kutoka visiwa vya komoro. (alama 2)

16. Zana hizi zimenunuliwa kwa bei ghali sana (alama 2)

Zana – kifaa chochote kitumiwacho na binadamu

Sana - kielezi

17. Utingo aliyeugua ametibiwa (alama 2)

18. amri

Ombi/ rai (alama 2)

19. hamaki/ ghadhabu

Kiamboni, mastakimuni, chengoni. (alama 2)

**SEHEMU YA D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

1.Sajili ya mtaani/sajili ya vijana. (Alama 2)

2.Sifa za sajili ya mtaani. (Alama 4)

(i)Ni lugha legevu

(ii)Huchanganya ndimi

(iii)Hutumia misimu kwa wingi

(iv)Hukosa mada maalum

(v)Huwa na sentensi fupi

(vi)Kuna kukatizana kauli

(vii)Kuna matumizi ya sheng'

3.Dhima ya lugha (Alama 4)

(i)Mawasiliano

(ii)Ni chombo cha kujieleza na kutoa mawazo

(iii)Huleta ushirikiano katika jamii

(v)Huburudisha

(vi)Ni kitambulisho cha jamii

(vii)Hutatua mizozo

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke
Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(viii)Huhifadhi utamaduni

**SEHEMU YA E :FASIHI SIMULIZI** ( ALAMA 15)

1.(i)Bembelezi /Bembea/Pembejezi (Alama 1)

(ii) Sifa za Bembelezi

(a)Huimbwa kwa taratibu kwa sauti ya hadhi ya chini.

(b)Huimbwa na wazazi au walezi

(c)Huwa fupi

(d)Hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine

(e)Huimbwa kwa kurudiarudia maneno

(f)Hutumia lugha shawishi

2.(i)Kipera

Kipera ni utungo unaowasilishwa kwa hadhira.

(ii)Lugha

Lugha ni malighafi ya fasihi simulizi (Alama 2)

3.(i)Hurafa

Hadithi ambazo huwa na wahusika wanyama pekee wanaowakilisha sifa za binadamu.

(ii)Mighani

Hadithi za mashujaa (Alama 2)

4.Umuhimu wa vitendawili (Alama 4)

(i) Huelimisha

(ii)Huburudisha

(iii)Hufundisha kaida na maadili ya jamii

(iv)Hukuza ubunifu na stadi ya kufikiria haraka

(v)Hukuza uwezo wa kukumbuka

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes
Teacher.co.ke

(vii)Hutambulisha jamii

(viii)Huchochea tabia ya udadisi

(ix)Hukuza na kusambaza ujuzi wa lugha

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes